

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA
MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA MAALUM LA MADIWANI KWA AJILI
YA KUJADILI HOJA ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA
SERIKALI (CAG) KILICHOFANYIKA
TAREHE 14/08/2017

MAHUDHURIO

1. MH. ERICK E. NKILAMACHUMU	MWENYEKITI
2. MH. JOHN M. SHIM' IMANA	MJUMBE
3. MH. MKUBILA S. SOUD	MJUMBE
4. MH. ADRONIZI E. BURINDOLI	MJUMBE
5. MH. OLIPA A. BUGOKE	MJUMBE
6. MH. KHAMIS HAMADI B.	MJUMBE
7. MH. JUSTUS K. MASUMO	MJUMBE
8. MH. DAVID I. BUZUTU	MJUMBE
9. MH. GWIHANGWE M. EDWARD	MJUMBE
10. MH. VAILETH MADENDE	MJUMBE
11. MH. SAID R. SOUD	MJUMBE
12. MH. ZAWADI D. COSMAS	MJUMBE
13. MH. WILBARD J. BAMBARA	MJUMBE
14. MH. GWASSA NTUNGIYE	MJUMBE
15. MH. SUZANA N. BAHATI	MJUMBE
16. MH. FIDEL F. NDANGWA	MJUMBE
17. MH. MUKIZA S. BYAMUNGU	MJUMBE
18. MH. NZEYE LEONARD	MJUMBE
19. MH. SENTORE J. MIBURO	MJUMBE
20. MH. PHILBERT M. KIIZA	MJUMBE
21. MH. MUGATA M. ELIAS	MJUMBE
22. MH. GEORGIA MUNYONYELA	MJUMBE
23. MH. KAGOMBA S. GEORGE	MJUMBE
24. MH. LAURENT J. MUSUNGALELE	MJUMBE
25. MH. CATHERINE EDWARD	MJUMBE
26. MH. JOHN E. RUZIGE	MJUMBE
27. MH. REHEMA S. RAMADHANI	MJUMBE
28. MH. SAFARI M. BANIGWA	MJUMBE
29. MH. EDITHA MWINURA	MJUMBE
30. BW. AIDAN J. BAHAMA (DED)	KATIBU

WAJUMBE WASIOHUDHURIA

Hakuna

WAGENI WALIOALIKWA:

- | | |
|---------------------------------------|-----------------------------|
| 1. MEJ. GEN. (MSTAAFU) SALUM M. KIJUU | RC - KAGERA |
| 2. CP. DIWAN ATHUMAN | RAS – KAGERA |
| 3. LT. CON. MICHAEL M. MNTENJELE | DC - NGARA |
| 4. Bw. HUDSON BAGEGE | M/KITI - CCM (W) |
| 5. BI. MWAJEMI BALAGAMA | KATIBU - CCM (W) |
| 6. BW. DAVID R. LYAMBOKO | AAS – RAS |
| 7. BW. VEDASTUS TIBAIJUKA | DAS – NGARA |
| 8. BW. PIUS NGAIZA | FMO |
| 9. BW. LEOPOLD NGIRWA | IA – LGA |
| 10. BW. JEREMIA M. KISIRI | CAG |
| 11. BW. KILILIMBI M. MWIKOLA | CAG |
| 12. BW. SYLVESTER RAPHAEL | DPS |
| 13. BW. CATHBERT THADEO | MWANDISHI WA HABARI – TBC |
| 16. BW. SHAABAN NDYAMUKAMA | MWANDISHI WA HABARI – RK |
| 17. H1813 PC. ATHUMAN HUSSEIN | ADC- RE – KAGERA |
| 18. H1852 PC. HAMZA RANGE | ADC – RAS – KAGERA |
| 20. INNOCENT RWEZAULA | MWANDISHI WA HABARI AZAM TV |

WATAALAM WALIOHUDHURIA:

- | | |
|------------------------------|---------------------|
| 1. BW. BURILO M. DEYA | MWANASHERIA |
| 2. BW. JULIUS ERNEST | Ag. DO - NYAMIAGA |
| 3. BW. WILFRED MAGIGE | DCSQA |
| 4. BW. RUKIZA ABED | ICTO |
| 5. BW. SELIALIS ANTHONY | TEO –RULENGE |
| 6. BW. REUBEN KYAMANI | Kny. DT |
| 7. BW. PASTORY M. MSABILA | DO – MURUSAGAMBA |
| 8. BW. MUZORA E. BITESIGIRWE | DHRO |
| 9. BW. GIDEON S. MWESIGA | DPEO |
| 10. DR. REVOCATUS NDYEKABORA | DMO |
| 11. BW. CONSTANTINE MUDENDE | DAICO |
| 12. BW. MORIS MOMBIA | DO – RULENGE |
| 13. BI. KALENZO S. MAJANJA | S/O |
| 14. BW. JAWADU YUSUPH | DO - KANAZI |
| 15. BW. FELICIAN M. KAPAMA | DIA |
| 16. BW. SANGATATI JOSEPHAT | DLFO |
| 17. BW. HERMAN HUME | DCDO |
| 18. BW. MARTON JAMES | Kny. DSEO |
| 19. BW. ROBERT ASSA | Kny. MENEJA WA MAJI |
| 20. BI. MARIAGORETH AUGUSTIN | KATIBU WA AFYA |

21. BW. PATRICK A. OGO	DPHAM
22. BI. GODLIVER J. GWAMBASA	DWE
23. BW. SYPRIANI G. MUHELANYI	Ag. DPLO
24. BI. PATRICIA R. SHAKANYI	Ag. DE
25. BI. JASMIN PETER	Ag. EO
26. BI. BETTY S. MUNUO	DLNRO
27. BW. ZAWADI N. WAZIRI	Ag. DEMO
28. BW. ODHIAMBO Y. AZARIA	DHO
29. BI. REGINA J. SOLOMA	HHS
30. BW. SAID SALUM	AFISA UTAMADUNI
31. BW. MASATU CHISUMO	SLO
32. DR. NGOWI R. S	DVO
33. BW. EZRA G. SASAGRE	Ag. TEO
34. BI. VIVIAN M. MARUHE	MUB
35. BI. DORAH BYAMUNGU	M/MAPATO
36. BW. STEPHANO D. NGULINZIRA	MWANDISHI WA VIKAO

MUHT.NA.01/2017/2018: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti aliwakaribisha ukumbini viongozi kutoka Mkoani, Wajumbe na Wataalam kwa kuwasalimia na kisha kuomba ridhaa ya Mkuu wa Mkoa ili Kikao kiweze kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aliwaomba Wajumbe wasimame kwa muda wa dakika moja kwa ajili ya kuwa kumbuka na kuwaombea marehemu waliofariki dunia ambao ni marehemu Mh. Roman Mitabaro Diwani wa Kata ya Keza , marehemu Alfred K. Katenga Afisa Elimu ya Sekondari na marehemu Owden M. Mbuba Afisa Utawala na Utumishi (W). Baada ya kutamka hayo Kikao kilifunguliwa saa 5:12 Asubuhi.

Baada ya ufunguzi wa Kikao Mwenyekiti alimkaribisha Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Ngara ili amkaribishe Mh.Mkuu wa Mkoa.

Mkuu wa Mkoa alianza kwa kuwasalimia Wajumbe pamoja na wataalam, na kueleza kuwa lengo la Kikao ni kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Aidha alieleza kuwa atapenda kujua utekelezaji wa maagizo aliyoyaacha kwenye Kikao kilichopita juu ya kuwachukulia hatua watumishi waliobainika kusababisha uzembe.

Pia alishauri Halmashauri ya Wilaya ibadili utaratibu wa kujibu hoja za CAG ili i isiendelee kupata hati zenye mashaka.

- i. Katika ukaguzi wa mwaka 2015/2016 Mfuko wa Basketi Fund kulikuwa na hoja ya manunuzi ya dawa yenye thamani ya Tshs.54,937,500/= kutoka maduka ya Dawa ya watu binafsi, hivyo alitaka kujiridhisha kama hoja hiyo ilitekelezwa kwa kuwataka Mkurugenzi Mtendaji (W), Mganga Mkuu (W) na Afisa Ugavi wathibitisha hilo kwa kuonyesha kibali kutoka MSD ili hoja hiyo

iweze kufungwa. Wataalam kutoka Mkoani walijiridhisha kwa kukagua viambatisho na hoja ilifungwa.

- ii. Manunuzi ya vifaa tiba vyenye thamani ya Tshs. 9,591,700/=, Mkuu wa Mkoa aliwataka Mkurugenzi Mtendaji (W), Mganga Mkuu (W) na Mfamasia waonyeshe viambatisho ili hoja hiyo iweze kufungwa.

Mfamasia alieleza kuwa baada ya kufuatulia ilibainika kuwa manunuzi hayo yalitumia Mfuko wa Basket na Fedha iliyomo inatakiwa MSD wahamishe Fedha kutoka kwenye akaunti yao na kuletwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi mtendaji pia alitoa utaratibu uliotumika. Aidha CAG Mkoa alieleza kuwa manunuzi ya dawa hizi hayakupokelewa kwani Invoice ilikuwa tofauti.

Mfamasia alishauri kuwa apewe muda ili nyaraka zilizohusika ziweze kuonyeshwa kama ushahidi.

Ushauri wa Mkoa hakuna muda maana hoja hii ni ya muda mrefu hivyo kilicho baki ni watu kuwajibishwa.

Kama kuna ushahidi nyaraka ziletwe ili ziweze kupitiwa na wakuguzi wa Mkoani.

- iii. Upotevu wa nyaraka za malipo ya Tshs. 24,279,189/= malipo ya 2015/2016 Mfuko wa Afya.

Mh.Mkuu wa Mkoa aliagiza Mkurugenzi Mtendaji (W), Mhasibu wa Afya (Gladys Samugabo) wawasilishe nyaraka hizo maana siku 90 zilizotolewa tangu Julai 2017 zilikwisha. Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa nyaraka hizo zilishawasilishwa kwenye Kitabu chenye vielelezo. Aidha ilielezwa kuwa Gladys ni Cashier na siyo Mhasibu wa Afya.

- iv. Ukaguzi wa 2014/2015 kutopeleka vifaa tiba kwenye zahanati ya Munjebwe na Mumuhamba, Vitanda 2.

Waliombwa Mkurugenzi Mtendaji (W), Mganga Mkuu (W) na Katibu waq Hospitali kuwasilisha nyaraka husika za mapokezi ya vifaa hivyo, Mganga

Mkuu (W) alieleza kuwa vitanda vilishapelekwa hivyo kwa vile hakupewa muda wa kuandaa nyaraka hizo aliomba kupewa muda wa kuziandaa.

Mhe. Diwani wa Rulenge alieleza kuwa vitanda vipo katika zahanati ya Munjebwe ila hawezi kubaini ni vya mwaka gani maana havikuandikwa Mwaka wa mapokezi.

Naye Mhe. Diwani wa Kata ya Kibogora alithibitisha kuwa, Kitanda kipo, na Mhe. Mwenyekiti alithibitisha katika zahanati ya Mumuhamba kitanda kilipelekwa pia aliomba Wah. Madiwani wawe wanapewa taarifa ya vifaa vinayopelekwa kwenye zahanati zao.

Azimio: Mganga Mkuu (W) apeeke Issue Voucher na Delivery Note ifikapo tarehe 15/08/2017 ili hoja ifungwe.

Katibu Tawala (M) aanzishe utaratibu wa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mkuu wa Mkoa juu ya watumishi wanaochelewesha utekelezaji wa maagizo

- v. Manunuzi ya vifaa tiba vyenye thamani ya Tshs.67,554,000/= bila stakabadhi ya EFD Mashine kutoka kwa wauzaji binafsi

Mh.Mkuu wa Mkoa alihoji juu ya gharama kubwa za kudurufu nyaraka kwenye Idara ya Elimu zaidi ya Tshs. 34,000,000/= kwa nini wasinge nunua mashine?

Azimio: Tarehe 21/08/2017 zionekane Risti za EFD Mashine toka kwa wazabuni wote ambako manunuzi yalifanyika.

Wakurugenzi Watendaji wote Mkoa wa Kagera wawatake watoa huduma wawasilishe ristiza EFD's, Wakuu wa Wilaya, Meneja wa TRA wachukue hatua kwa wahusika wote walio wasaidia wafanya biashara kukwepa ushuru suala hilo lisimamiwe kikamilifu.

Mh.Mkuu wa Mkoa alitoa maagizo yafuatayo:

- i. Kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 taarifa zote za Mkaguzi wa ndani kila Robo zionyeshe huduma iliyotolewa pamoja na risti za EFD Mashine.
- ii. Halmashauri itakayokuwa na hoja za manunuzi yasiyo kuwa na risti za EFD Mashine mhusika atachukuliwa hatua, hivyo Makatibu Tawala (W) na Katibu Tawala (M) waanze kuchukua hatua kwa mamlaka waliyopewa.

Aidha Mh.Mkuu wa Mkoa alihoji juu ya thamani ya mali za Halmashauri kuwa ni bilioni 3; hivyo alishangaa na kueleza kuwa mali za Halmashauri

hazipungui bilioni chini ya 100 kwa kuanza alitoa mfano wa miradi ya Maji kuwa ina thamani kubwa, Shule moja ya Sekondari ina thamani ya milioni 500.

Alihoji wathamini waliokodiwa kuja kufnaya kazi ya uthamini wanafanya kazi gani.

Mwenyekiti alieleza kuwa mpaka sasa wathamanishaji mpaka leo hii wapo kazini wanaendelea na kazi ya uthamanishaji na hawajakamilisha, hivyo alikanusha taarifa iliyotolewa kuwa siyo sahihi. Aidha Mkurugenzi mtendaji alieleza kuwa taarifa hiyo ni ya miaka ya nyuma.

- vi. Upotevu wa vitabu 9 vya kukusanyia mapato ya ndani. Alihoji kwa nini hadi leo hii hakuna hatua za kinidhamu zilizokwisha chuliwa kwa wahusika?.

Azimio: Mkurugenzi Mtendaji (W) achukuwe hatua ya kuwasimamisha kazi wahusika wote na ndani ya siku tatu (3) wawe wameonyesha vitabu hivyo kama itashindikana taratibu za kuwaondoa kweye Utumishi zifuate.

- vii. Matumizi ya Fedha za miradi kinyume na maagizo ya Bunge.Tshs. 263,763,994/= miradi ya maji vijijini

Agizo: Fedha zote zilizotumika isivyo ziwe zimerejeshwa ifikapo tarehe 30/09/2017 kwa Wilaya zote Mkoa wa kagera ili shughuli zilizokuwa zimepangwa zitekelezwe.

- viii. Fedha za mkopo Ngara Vijana SACCOS Tshs. 15,000,000/= ambazo Vijana walifanya ubadhilifu.

Kuhusu hoja hiyo, Mwenyekiti alieleza kuwa zimerejeshwa milioni 7 bado milioni 8 na kesi bado ipo Mahakamani, aidha alieleza kuwa Mwanasheria wa Halmashauri hatoi taarifa ya mwenendo wa kesi, pia aliomba mhusika wa ubadhilifu achukuliwe hatua.

Mh. Mbunge alieleza kuwa kupitia vikao vya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango Mwanasheria aliagizwa kufuatilia nakala ya hukumu lakini taarifa haitolewi, pia Mkurugenzi Mtendaji (W) hakushirikishwa katika kukata rufaa wakati yeye ndiye mlalamikaji.

Aidha Afisa Sheria (W) alieleza kuwa kesi iliombewa rufaa kwa pande zote mbili, hivyo aliomba kufatilia na atawasilisha taarifa .

ix. Tshs. 84,347,887/= kutopelekwa katika Mfuko wa wanawake, Mh.Mkuu wa Mkoa aliomba maelezo ya Mkurugenzi Mtendaji (W) na Afisa Maendeleo ya Jamii (W) kwanini hawakutekeleza maelekezo ya Serikali ya kutenga asilimia 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Vikundi vya Vijana na Wanawake.

Azimio: Tarehe 25/08/2017 yapelekwe maelezo kwa kwa Mh.Mkuu wa Mkoa juu ya mapato ya Halmashauri na jinsi walivyo changia vikundi vya vijana na wanawake.

x. Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato katika Mfumo wa LGRCIS vyanzo vyote vya mapato, ushuru wa magulio, miradi n.k vyote viingizwe katika mfumo wa mahine za POS ili kubaini mapato yote yanayo kusanywa.

Agizo: Katibu Tawala (M) andae utaratibu wa kupata taarifa za POS zote katika Mkoa wa Kagera ili kufahamu mapato yanayokusanywa, mashine za POS zisizotumika ili Mkurugenzi husika afahamishwe.

Azimio: Mkurugenzi Mtendaji (W) ahakikishe hoja zote za maagizo ya Bunge zinajibiwa pamoja na vielelezo viwepo ili hoja hizo ziweze kufungwa mwisho wa mwezi huu kabla ya kufanyika kwa MOCK LAAC.

Katika kuhitimisha mjadala wa hoja Mh.Mkuu wa Mkoa alitoa ushauri ufuatao:

- Mkurugenzi awatumie vizuri wakaguzi wa ndani na Kamati za ukaguzi ziweshwe ili zifanye kazi vizuri.
- Vibuniwe vyanzo vingine vya mapato ili kupandisha mapato ya Halmashauri ya Wilaya.
- Wah. Madiwani wafuatilie Miradi na kuhakikisha inakamilika kwa wakati na itekelezwe kwa kiwango.
- Asilimia 10% ya Vikundi vya Vijana na Wanawake isimamiwe na kuhakikisha Vikundi hivyo vinapelekwa Fedha na visimamiwe ili kujiridhisha kama shughuli zao zinaendelea vizuri.
- Vichaguliwe Vikundi vichache vinavyofanya vizuri vipewe Fedha nyingi ili kuendeleza shughuli zao.

Mwisho hatua zichukuliwe kwa watu wanaosababisha hoja, waitwe na wapewe muda maalum wa kutekeleza hilo na ikishindikana wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Aliahidi kurudi Ngara baada ya miezi sita (6) ili kuona utekelezaji wa hoja hizo na aligiza kutoona tena hoja za miaka ya nyuma. Aliwashukuru Wajumbe na kuwatakia baraza njema.

Mwenyekiti alimshukuru Mh.Mkuu wa Mkoa kwa maelekezo aliyoyatoa na kusema kuwa, yeyote atakaye zembea na kusababisha hoja atachukuliwa hatua za kinidhamu. Hivyo Wajumbe walifiki kuwa Mh. Mkuu wa Mkoa arudi mwezi Februari 2018 kujiridhisha kama hoja za miaka ya nyuma zitakuwa zimetekelezwa.

NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA MH. MBUNGE

Kwanza, alishukuru ujio wa Mh. Mkuu wa Mkoa katika Kikao hicho.

Alieleza kuwa miongoni mwa vyanzo vya mapato vya kuongeza mapato ya Halmashauri ni mapoja na hifadhi za Taifa za Burigi na Kimisi kupitia vitalu vya uwindaji.

Pia Halmashauri inajipanga kuwasiliana na Ofisi mbalimbali za Serikali ili kuanzisha utalii wa ndani kutokana na vivutio vilivyopo Ngara. Alisisitiza kuwa asilimia 10% ya Vikundi vya Vijana na Wanawake maelekezo ya Serikali yasipozingatiwa bado hoja zitazidi kuwepo.

Uhamisho wa Watumishi bila kulipa stahiki zao nalo linaweza kuleta hoja, hivyo Katibu Tawala (M) aangalie suala hilo kwa Wilaya zote za Mkoa wa Kagera.

NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA MH. MWENYEKITIWA CCM (W)

Alimshukuru Mh. Mkuu wa Mkoa kwa utaratibu alio utumia katika kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alikemea suala la kutokukamilisha taarifa kwani hili hupelekea wilaya kuwa na hati yenye mashaka.

Pia alimuomba Mh. Mkuu wa Mkoa atoe majibu kuhusiana na Ngara Farmers kuhusu madeni yanayodaiwa na hatua zilizochukuliwa maana suala hili lilishafikishwa kwenye Ofisi yake.

Mwisho, alishukuru kazi zinazofanywa na Wah. Madiwani pamoja na wataalam katika kusimamia Maendeleo ya Wilaya ya Ngara.

NENO LA SHUKRANI KUTOKA KWA MKURUGENZI Mtendaji (W)

Alimshukuru Mh.Mkuu wa Mkoa kwa ushauri,maelekezo na maagizo mbalimbali na kuahidi kuyafanyia kazi ili hoja za zamani ziweze kufungwa. Pia Menejimenti inakwenda kuongeza vyanzo vya mapato ambapo alieleza kuwa kazi hiyo ilishafanyika, kilichobaki ni kuvichambua.

MUHT.NA.2/2017/2018: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alimpongeza Mh.Mkuu wa Mkoa kwa jinsi alivyoendesha Kikao, alisisitiza Mkurugenzi Mtendaji na Watalaam wawasilishe viambatisho vinavyohitajika ili hoja za zamani ziweze kufutwa. Baada ya kutamka hayo Kikao kilifungwa waa 7:20 Mchana.

UMETHIBITISHWA

.....

Mh.Erick E. Nkilamachumu

MWENYEKITI

.....

Bw.Aidan J. Bahama

KATIBU

TAREHE...../...../2017